# <u>Maagizo ya Kusanidi Campus Parent</u>

**Mzazi:**
**Simu:**
**Barua pepe:**
**Uhusiano:**

**<u>MUHIMU</u>: <u>Wazazi/Walezi watahitaji kufungua akaunti yao ya tovuti ya CAMPUS PARENT ili kuangalia maelezo ya usafirishaji wa mtoto wao, kutuma ombi la kupata chakula cha mchana bila malipo na bei iliyopunguzwa, kadi ya ripoti, mahudhurio, gredi, kazi na matokeo ya mtihani.</u>**

Ikwia tayari umesanidi akaunti yako ya Francis Howell Campus Parent, tafadhali puuza barua hii. Hii sio ya akaunti ya CAMPUS STUDENT.

Hapa chini utapata "Ufunguo wako binafsi wa Kuwezesha', ambao utakuruhusu kufungua Akaunti yako mwenyewe ya Campus Parent Portal kwa Wilaya ya Shule ya Francis Howell. Tunatumainia kwamba Campus Parent itakuwa zana muhimu kukusaidia kufuatilia maendeleo ya kielimu ya mtoto wako.

**<u>UFIKIAJI WA CAMPUS PARENT:</u>**

**Jina la Mwanafunzi:**

**Nambari ya Kitambulisho cha Mwanafunzi:**

**Gredi:**

**Activation Key (Ufunguo wa Kuwezesha):**

**Je, Campus Parent ni nini?**

> Campus Parent ni zana yetu ya wazazi kufikia maelezo ya mwanafunzi haraka, mtandaoni na kwa njia salama ikijumuisha: usafirishwaji, kutuma maombi ya faida za chakula, ratiba za masomo, kazi, mahudhurio, nidhamu, usajili wa kozi kwa mwaka ujao, kadi za ripoti na matokeo ya mtihani.
>
> Campus Parent ni njia ya kukuza zaidi ubora wa kielimu kwa kuboresha mpango wetu wa mawasiliano wa pamoja na wazazi na wanafunzi.

**Je, ni nani anastahiki kuwa na akaunti ya Campus Parent?**


> Wazazi au Walezi wa mwanafunzi aliye shuleni ndio wanastahiki kuwezesha akaunti ya Campus Parent, baada ya kukubaliana na sheria na masharti ya matumizi. Wilaya hufungua akaunti za Campus Student otomatiki kwa kila mwanafunzi anayetumia FHSD. Akaunti za wanafunzi huwaruhusu kufuatilia tu maelezo yao **<u>wenyewe</u>**, bali akaunti za wazazi hufikia maelezo ya watoto wao **<u>wote</u>** walioandikishwa wilayani.


**Je, ni wapi ninaweza kupata maelezo zaidi kuhusu Campus Parent au Campus Student?**

Utapata maelezo zaidi kwenye kurasa za wavuti za Shule na Wilaya chini ya Tovuti ya Campus

***Using the GUID/Activation Key to Create Usernames and Passwords (Ukitumia GUID/Ufunguo wa Kuwezesha ili Uunde Majina ya mtumiaji na Nenosiri):***

**Ufunguo wa Kuwezesha** unahitajika tu watumiaji wa mara ya kwanza wanapofikia tovuti kusanidi akaunti yao. Nenda kwenye ukurasa wa **Campus Parent Login**:
https://francishowellmo.infinitecampus.org/campus/portal/parents/francis.jsp
Ikiwa lugha nyingine inahitajika, bofya kwenye chaguo chini ya kidirisha, chaguo la lugha limedhibitiwa kwa wakati huu.




Chini ya skrini ya kuingia kwenye akaunti, utaona "New User"?

1. Chaguo hili hutumika **tu** kwa mara ya kwanza unapofikia na kusanidi akaunti yako ya Campus Parent.
2. Weka ufunguo wa kuwezesha wa herufi 32 uliopewa kisha chagua **Submit.**
3. Ufunguo wa kuwezesha utathibitishwa na kisha kuonyesha skrini ya kuunda **Username (Jina la Mtumiaji)** na **Password (Nenosiri)**.
4. Weka **Username (Jina la Mtumiaji)** ambalo ni spesheli na lililo na urefu wa angalau herufi 5.
5. Weka **Password (Nenosiri)**. Ni vyema kutumia nenosiri la alfanumeriki (herufi na nambari) ambalo lina urefu wa angalau herufi (8).
6. Weka nenosiri kwa mara ya pili katika eneo la **Verify Password (Thibitisha Nenosiri)**.
7. Bofya kitufe cha **Create Account (Unda Akaunti)**.
8. Weka **security email address (anwani ya usalama ya barua pepe)** kisha uweke tena nenosiri yako mpya ya tovuti.

**Kumbuka:** Ukisahau jina la mtumiaji na nenosiri yako, barua pepe iliyo na kiungo itatumwa kwa anwani hii ya usalama ya barua pepe ili ikusaidie kuzirejesha.


**Kwa watumiaji ambao wamewezesha Campus Parent yao, lakini wamesahau nenosiri yao au jina la mtumiaji:**

- Bofya kwenye **Forgot Username (Nimesahau Jina la Mtumiaji)?**

Weka anwani ya usalama ya barua pepe ya akaunti yako ili utumiwe barua pepe iliyo na jina lako la mtumiaji.

- Bofya kwenye **Forgot Password (Nimesahau Jina la Mtumiaji)?**

Weka jina lako la mtumiaji ili utumiwe kiungo cha kuweka upya nenosiri kwenye anwani ya usalama ya barua pepe ya akaunti yako kwenye faili.




Barua pepe itatoka kwa **infinitecampushelp@fhsdschools.org**.

Tafadhali angalia folda yako ya taka ikiwa hukuona barua pepe.

Ikiwa HUTAPOKEA barua pepe, unaweza kuwasiliana na FHSD Help Desk ili upate msaada wa kufikia akaunti yako kupitia help.desk@fhsdschools.org au 636-851-HELP (4357).

**Jaribu Apps za Campus Parent na Campus Student!**